**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**

**BUNGE LA TANZANIA**

# ORODHA YA SHUGHULI ZA LEO

## MKUTANO WA ISHIRINI

## KIKAO CHA THELATHINI NA SABA

**26 JUNI, 2015**

# ORODHA YA SHUGHULI ZA LEO

---

## MKUTANO WA ISHIRINI

### KIKAO CHA THELATHINI NA SABA – TAREHE 26 JUNI, 2015

## I. MASWALI:

### OFISI YA WAZIRI MKUU:

### 260. MHESHIMIWA DEOGRATIAS ALOYCE NTUKAMAZINA (NGARA):

- Atamuuliza Mheshimiwa Waziri Mkuu:- Mnamo Novemba, mwaka 2010 wakati Mheshimiwa Rais akizindua Bunge, pamoja na mambo mengine aliwaeleza Wananchi kuwa Serikali ingeanzisha mfuko maalum kwa ajili ya ujenzi wa Nyumba za Walimu nchi nzima:-

(a) Je, ni lini mfuko huo muhimu utaanzishwa;

(b) Je, ni lini Serikali itapunguza tatizo la nyumba za Walimu Wilaya ya Ngara yenye jumla ya Walimu wa Sekondari 312 na nyumba 67 tu, pamoja na Walimu wa Shule za Msingi 1437 ambapo nyumba zilizopo ni 292 tu na hivyo kuacha Walimu zaidi ya 1145 wasio na makazi.

**261. MHESHIMIWA MUSTAPHA BOAY AKUNAAY (MBULU):**

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri Mkuu:- Katika utaratibu wa ukusanyaji ushuru wa Serikali za Mitaa:-

(a) Je, Kukusanya ushuru bila huduma kutolewa kama vile kuwatoza akina mama ushuru wa eneo la wazi kwenye mnada ili wauze bidhaa zao kama vyungu, kamba nk inakubalika;

(b) Je, ni sahihi kutumia Polisi katika kukusanya ushuru.

**WIZARA YA MAWASILIANO, SAYANSI NA TEKNOLOJIA:**

**262. MHESHIMIWA RUKIA KASSIM AHMED (VITI MAALUM):**

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Mawasiliano, Sayansi na Teknolojia:- Vijana wa kike wanaojiunga na Chuo cha Dar es Salaam Insititute of Technology (DIT) ni wachache ikilinganishwa na vijana wa kiume:-

Je, Serikali ina mikakati gani ya kuhamasisha vijana wa kike kujiunga kwa wingi na Chuo hicho ili kuboresha uwezo wao na maisha kwa ujumla.

## WIZARA YA UJENZI:

**263. MHESHIMIWA MODESTUS DICKSON KILUFI (MBARALI):**

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Ujenzi:- Barabara ya Rujewa – Madibira – Mafinga ni kiungo muhimu kwa usafirishaji wa Mpunga na mazao mengine lakini barabara hiyo haina lami:-

(a) Je, ni lini barabara hiyo itajengwa kwa lami;

(b) Je, kwa nini ahadi ya Mhe. Rais kwa wananchi wa Mbarali ya kujenga barabara hiyo kwa lami haitekelezwi.

## WIZARA YA VIWANDA NA BIASHARA:

**264. MHESHIMIWA BETTY ELIEZER MACHANGU (VITI MAALUM):**

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Viwanda na Biashara:- Serikali imeruhusu Supermarkets za Uchumi na Nakumati zote za Kenya kuingia katika soko la Tanzania kuuza bidhaa zao zikiwemo za Mifugo kutoka nchini kwao lakini Wafanyabiashara wa Tanzania kama vile Azam, Konyagi ya Tanzania wauzaji wa Maziwa wa Tanzania wamekuwa wakizuiwa kuingiza bidhaa zao katika soko la Kenya:-

(a) Je, Serikali ina mikakati gani ya kulinda viwanda vyetu, Wakulima/ Wafugaji wetu kwa kuzuia uingizaji nchini wa bidhaa zinazozalishwa hapa nchini;

(b) Je, kwa nini Serikali inaruhusu maduka hayo kuajiri Watendaji (***Cashiers***) kutoka nchini kwao badala ya kuajiri watanzania.

## WIZARA YA FEDHA:

**265. MHESHIMIWA RAJAB MBAROUK MOHAMMED (OLE):**

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Fedha:-

Je, ni kwa namna gani Serikali kupitia vitengo vya Ukaguzi wa Ndani (Internal Audit) katika Wizara na Serikali za Mitaa vinajihusisha na Ukaguzi wa Miradi inayofadhiliwa na nchi wahisani.

## WIZARA YA KILIMO, CHAKULA NA USHIRIKA:

**266. MHESHIMIWA KAPT. JOHN ZEFANIA CHILIGATI (MANYONI MASHARIKI):**

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Kilimo, Chakula na Ushirika:- Wilaya ya Manyoni iko kwenye ukanda wa ukame hivyo hukabiliwa na upungufu wa chakula wa mara kwa mara na kuifanya Serikali kupeleka chakula cha msaada

wa njaa wakati kuna skimu saba (7) za umwagiliaji lakini kunakosekana Bwawa la kutoa maji kwa ajili ya skimu hizo:-

(a) Ipo site nzuri katika kijiji cha Bwasa inayofaa kwa ujenzi wa Bwawa hilo na upembuzi umekamilika; Je, Serikali ipo tayari kushirikiana na Wananchi wa Manyoni kuhakikisha Bwawa hilo linajengwa;

(b) Upembuzi yakinifu unaonyesha gharama ya ujenzi wa Bwawa hilo ni shs. bilioni 2.4; Je, Serikali ipo tayari kutenga fedha kwenye bajeti zijazo japo kwa awamu ili utekelezaji wa mradi huo uanze;

(c) Ujenzi wa Bwawa hilo utakwenda sambamba na ujenzi wa Skimu mpya ya Umwagiliaji katika kijiji cha Mwiboo wa hekta 400 na itagharimu sh. bilioni 1.7; Je, Serikali ipo tayari kutenga fedha za ujenzi wa skimu hiyo kupitia Mpango wa Matokeo Makubwa Sasa (BRN).

## WIZARA YA NISHATI NA MADINI:

### 267. MHESHIMIWA NYAMBARI CHACHA NYANGWINE (TARIME):

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Nishati na Madini:- Mgodi wa North Mara unaomilikiwa na Kampuni ya Barrick, sasa Acacia umekuwa ni kero kubwa na janga kwa wananchi wa Tarime:-

(a) Je, kwa nini Wananchi wa Nyamichale – Kijiji cha Nyakunguru waliofanyiwa tathmini na Serikali ili maeneo yao yachukuliwe na Mgodi hawajapatiwa malipo ya fidia;

(b) Kuna mauaji ya mara kwa mara kwa vijana wasio na hatia kwenye maeneo yanayozunguka Mgodi; Je, hadi sasa ni vijana wangapi waliouawa na askari wanaolinda Mgodi huo, na Serikali inashauri nini Wananchi wa Tarime juu ya tatizo hilo;

(c) Je, kwa nini mgodi umeshindwa kutekeleza ahadi za Maji, Elimu, Afya, barabara na Umeme katika vijiji saba vinavyozunguka mgodi.

**268. MHESHIMIWA IGNAS ALOYCE MALOCHA (KWELA):**

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Nishati na Madini:-

Je, ni lini Serikali itapeleka umeme katika Kata kumi na tatu zilizoko katika ukanda wa Ziwa Rukwa ambazo ni Mfinga, Mwadui, Kalumbaleza, Muze, Mtowisa, Izimba, Milepa, Ilemba, Nakankanga, Kapenta, Kaoze, Kipeta na Kilangawana.

## II. MISWADA YA SHERIA YA SERIKALI:

***(Kusomwa Mara ya Pili, Kamati ya Bunge zima na Kusomwa Mara ya Tatu)***

Muswada wa Sheria ya Vituo vya Pamoja Mipakani wa Mwaka 2015 *[The one stop Border Posts Bill, 2015]*

**DODOMA**<br>**26 JUNI, 2015**

**DKT. T. D. KASHILILAH**<br>**KATIBU WA BUNGE**